**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Simu:** +1 202-884-1080
+1 202-939-6125
**Nakushi:** +1 202-797-7408

**Baruapepe:** washington@nje.go.tz
ubalozi@tanzaniaembassy-us.org
**Tovuti:** www.us.tzembassy.go.tz

**1232 22nd Street, N.W.,
Washington, D.C. 20037.**

## TANGAZO

## FURSA ZA UFADHILI WA MASOMO KATIKA NGAZI YA SHAHADA YA UZAMILI *(MASTER'S DEGREE)*

Ubalozi unapenda kuwaarifu Watanzania kuhusu uwepo wa fursa za ufadhili wa masomo katika ngazi ya Shahada ya Uzamili *(Master's Degree)* kwa mwaka wa masomo 2026/2027 katika Chuo Kikuu cha Princeton, New Jersey na Chuo Kikuu cha Williams *(Williams College)*, Massachusetts.

### 1. CHUO KIKUU CHA PRINCETON

Chuo Kikuu cha Princeton kimetangaza kutoa ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili katika fani zifuatazo:

i. ***Master in Public Policy*** **(MPP); na**

ii. ***Master in Public Affairs*** **(MPA)**

❖ Vigezo vya Ufadhili:

- MPP – Ni programu ya mwaka mmoja (1) kwa waombaji wenye uzoefu wa kazi wa zaidi ya miaka saba (7+) *(mid-career applicants)*.
- MPA – Ni programu ya miaka miwili (2) kwa waombaji wenye uzoefu wa kazi wa kati ya miaka miwili (2) hadi minne (4) *(early career applicants)*.

🔗 Taarifa zaidi kuhusu fursa hizi zinapatikana kupitia tovuti: https://spia.princeton.edu/graduate-admissions

❖ Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **15 Desemba 2025**

### 2. CHUO KIKUU CHA WILLIAMS *(Williams College)*

Chuo Kikuu cha Williams *(Williams College)* kimetangaza nafasi za ufadhili wa masomo kwa mwaka wa masomo 2026/2027 katika fani ya **Master of Arts in Policy Economics *(MA in Policy Economics)*.**

Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/

❖ Vigezo vya Ufadhili:

Ufadhili huu ni kwa waombaji wenye uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu (3) katika masuala yanayohusiana na sera za umma.

🔗 Taarifa zaidi kuhusu fursa hii zinapatikana kupitia tovuti: www.cde.williams.edu

❖ Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **01 Desemba 2025**

Ubalozi unawahimiza Watanzania wenye sifa stahiki kuchangamkia fursa hizo.

**UBALOZI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NCHINI MAREKANI**
**WASHINGTON, D.C.**

**11 NOVEMBA 2025**

Created with Photo-to-PDF One Click Converter. Download here: https://firehawk.ai/phototopdf
https://firehawk.ai/phototopdf/